

**ENDESHA GARI KWA NJIA  
SALAMA KATIKA MICHIGAN**



**Mwongozo wa  
Wakimbizi**





# Yaliyomo

Utangulizi.....	4
-----------------	---

## Usalama wa Abiria

Mikanda ya Usalama .....	6
Watoto ndani ya Gari.....	6
Joto jingi mwilini .....	7
Kitanda cha Lori .....	7

## Mambo ambayo Yanaathiri Uwezo wa Kuendesha Gari

Matumizi ya Simu ya Mkononi .....	9
Kuvutwa mawazo Unapoendesha Gari.....	9
Watoto Kulewa .....	9
Kuendesha Gari Vibaya .....	10

## Sheria za Barabarani

Sheria ya “Songa Kando” .....	12
Mabasi ya Shule .....	12
Maeneo ya Ujenzi .....	13
Njia za Kusafiri.....	13
Ukiukaji wa Sheria za Kuendesha Gari.....	14
Mkataba wa Ukiukaji wa Trafiki .....	14
Kusimamishwa .....	15

## Maelezo ya Usimamizi

Usajili na Bima ya Gari .....	17
Leseni ya Michigan ya Kuendesha Gari .....	18
Leseni ya Mkimbizi ya Kuendesha Gari.....	19

Mwongozo huu unawapa wakimbizi maelezo kuhusu sheria za trafiki za Michigan na mazoea ya kuendesha gari vizuri. Mwongozo haujumuishi kila sheria ya trafiki ya Michigan. Umekusudiwa kama rasilimali kwa jamii ya wakimbizi ili kutoa ufahamu zaidi na kuimarisha usalama barabarani.



# Usalama wa Abiria

# Mikanda ya Usalama



- Sheria ya Michigan inawahitaji madereva, abiria wa mbele, na abiria wa nyuma wenyewe umri wa miaka 15 na wadogo kuvala mikanda ya usalama.
- Polisi wanaweza kusimamisha gari kama dereva au abiria wa mbele hawajafunga mikanda ya usalama.
- Mikanda ya usalama hukulinda ndani ya gari, ambayo hupunguza hatari ya kuumia sana au kifo katika ajali.
  - » Mifuko ya kinga imeundwa kufanya kazi pamoja na mikanda ya usalama.

**Mkanda wa bega**  
Mbali na shingo yako (lakini si mbali na bega lako)

**Kwenye kifua chako**  
Weka katikati ya matiti yako na uhakikishe umeondoaa kitu chocchte kinacholeea kwenye ukanda wako wa usalama

**Ukanda wa paja**  
Ifunge chini ya tumbo lako ili iweze kutosha vizuri kwenye mapaja na fupanyonga yako.

**Wanawake wajawazito wanapaswa kwa kawaida kuifunga juu, wakitumia ukanda wa bega na ukanda wa paja chini ya tumbo na kwenye nyong'a.**

## Watoto ndani ya Gari



- Sheria ya Michigan inawahitaji watoto kufungwa kwenye kiti cha gari au kiti cha nyongeza hadi angalau umri wa miaka 8 au urefu wa 4'9" (cm 144.78).
  - » Watoto huwa hawatoshei katika mikanda ya usalama na wanahitaji viti vya gari vya kuwalinda.
  - » Watoto wanapaswa kuwa katika kiti cha nyuma cha gari hadi kufikia umri wa miaka 2 na kisha kutumia kiti cha gari cha kuunganisha hadi umri wa miaka 5, wakati ambapo kiti cha nyongeza kinahitajika.
- Imepigwa marufuku kunyonyesha mtoto wakati gari linaendeshwa.
- Wakati unanunua kiti cha gari, usitumie ikiwa:
  - » Kiti kimehusika katika ajali hapo awali.
  - » Muda wa kiti kutumika umekwisha.
  - » Historia ya kiti haijulikani kwako (iwapo kilinunuliwa katika mauzo ya gereji au kwenye duka ya kuuzwa tena).

**Ambatisha kamba ya juu kwenye amari ya juu**

**Kaza viambatisho vya chini kwenye amari za chini**

## Joto jingi mwilini



- Usiache mtu ye yote, hasa mtoto, mtu mzee, au mnyama, peke yake ndani ya gari.
  - » Gari lenye joto linaweza kusababisha jeraha kali au kifo, na inaweza kusababisha dereva kutiwa mbaroni au kufungwa jela.
- Kwa dakika 10, joto la gari linaweza kuongezeka zaidi ya 20°F (11°C).
- Hata katika hali ya hewa ya 60°F (15.5°C), joto ndani ya gari linaweza kufikia 110°F (43.3°C).

## Kitanda cha Lori



- Hata kwa kasi ya chini, kubebwa kwenye kitanda cha lori, kikiwa kimefunikwa au wazi, ni hatari.
  - » Hakuna kitu cha kukulinda kwa tukio la ajali.
  - » Matuta au vizingo vya barabarani vinaweza kusababisha abiria kutupwa kutoka kwenye kitanda cha lori.
- Watu wenye umri wa miaka 18 hawawezi kubebwa kwenye kitanda kilicho wazi cha lori kwa kasi zaidi ya maili 15 kwa saa (kilomita 24 kwa saa) kwenye barabara ya umma.
  - » Hii haifai kwa gari linalodibitiwa au kuendeshwa na mwajiri au mfanyakazi wa kazi za shamba, biashara ya ujenzi, au biashara sawa wakati wa shughuli za kazi.



# Mambo ambayo Yanaathiri Uwezo wa Kuendesha Gari

## Matumizi ya Simu ya Mkono



- Sheria ya Michigan inakataza kusoma, kuandika kwa kutumia mikono, au kutuma ujumbe mfupi wakati unaendesha gari.
  - » Madereva wanaweza kupiga simu na kutumia vifaa vya GPS vilivyowekwa kwenye gari, lakini tabia hii ya kuvuta mawazo inapaswa kuepukwa, iwezekanavyo.
  - » Miji, vijiji, na nchi zinaweza kuweka sheria inayopiga marufuku kupiga simu katika mamlaka yao. Sheria hizi zitabandikwa wakati unaingia katika eneo hilo.
- Faini ya kosa la kwanza la kutuma ujumbe wakati unaendesha gari ni angalau \$100.

## Kuvutwa mawazo Unapoendesha Gari



- Madereva ambao wanavutwa mawazo na kufanya kosa la ukiukaji wa trafiki wanaweza kupokea tiketi.
- Mifano ya kuvutwa mawazo unapoendesha gari inaweza kujumuisha:
  - » Kutumia simu ya mkononi au kutuma ujumbe.
  - » Kula na kunywa.
  - » Kujipamba.
  - » Kusoma, pia ramani.
  - » Kutumia mfumo wa urambazaji.
  - » Kutazama video.
  - » Kubadilisha kituo cha radio, CD, au MP3.

## Watoto Kulewa



- Ni kinyume cha sheria kwa watu wenyewe umri wa chini ya miaka 21 kuwa na pombe.
  - » Watu wenyewe umri wa chini ya umri wa miaka 21 hawawezi kununua au kunywa pombe.
- Ni kinyume cha sheria kununua au kupea pombe watu wenyewe umri wa miaka 21.
  - » Watu wazima wanawajibika kisheria ikiwa mtu chini ya umri wa miaka 21 anakunywa pombe nyumbani kwake.
- Ni kinyume cha sheria kwa watu walio chini ya umri wa miaka 21 kuendesha gari wakati ameleta katika kiwango chochote.
- Wakati unaendesha au kubebwa ndani ya gari, usimiliki au kusafirisha pombe kwenye kontena iliyo wazi au isiofungwa.

## Kuendesha Gari Vibaya



- Usitumie gari ukiwa umelewa, umetumia dawa za kulevy, au kitu kingine chochote cha kulevy cha ambacho huzuia uwezo wako wa kuendesha gari.
  - » Dereva huchukuliwa kuwa amelewa akiwa na kiwango cha pombe kwenye damu cha .08 au zaidi.
  - » Dereva anaweza kutiwa mbaroni kwa kiwango chochote cha pombe kwenye damu ikiwa polisi anaamini anaendesha gari wakati amelewa.
  - » Kukataa kutekeleza kipimo cha kemikali kutafanya leseni kusitishwa kwa muda.
- Adhabu ni za juu ikiwa umepatikana na hatia ya kuwa na kiwango cha pombe kwenye damu cha .17 au zaidi.
- Hukumu ya kufanya kazi wakati umelewa inaweza kusababisha:
  - » Leseni kusitishwa kwa muda.
  - » Kuwekwa kwa kifaa cha kuzuia gari kuwashwa.
  - » Gari kuzuiwa.
  - » Kunyang'anywa nambari ya gari.
  - » Kunyimwa usajili wa gari.
- Wakosaji wanaweza pia kupata pointi kwenye leseni ya kuendesha gari, faini kubwa, kufungwa jela, na mipango ya lazima ya matumizi ya pombe. Adhabu ni kali zaidi kwa madereva wenye hatia za awali, hata kama ni za jimbo au nchi nyingine.
- Wakati unaendesha au kubebwa ndani ya gari, usimiliki au kusafirisha pombe kwenye kontena iliyo wazi au isiofungwa.



A photograph showing the back of a child wearing a dark jacket and a light blue backpack with white stripes. The child is walking away from the camera towards a white school bus. A stop sign is visible on the side of the bus.

# Sheria za Barabarani

## Sheria ya “Songa Kando”



- Kwa magari ya dharura yenyе taa zinazomweka:
  - » Nenda kwenye upande mmoja wa barabara, au
  - » Punguza mwendo na upite kwa uangalifu ikiwa barabara haitumiki.
- Kukosa kusonga kando ni pointi nne kwenye leseni ya kuendesha gari na angalau faini ya \$150.
- Aina ya magari ya dharura yanajumuisha:
  - » Magari ya polisi.
  - » Malori ya kuzima moto.
  - » Magari ya wangojwa na magari ya uokoaji.
  - » Malori ya kuvuta.
  - » Magari ya huduma.



## Mabasi ya Shule



- Shughulikia mabasi ya shule kama ishara za trafiki.
  - » Hakuna taa (kijani) = endelea vizuri.
  - » Mbele inawaka rangi ya manjano = jitayarishé kusimama.
  - » Mbele inawaka rangi ya nyekundu = simama.
- Simama angalau umbali wa futi 20.
  - » Magari katika njia zote mbili za usafiri lazima zisimame.
  - » Magari upande wa pili wa barabara kuu hayapaswi kusimama.
- Punguza mwendo kwenye au karibu na shule na maeneo ya makazi ambapo watoto wanaweza kuwa wanacheza.
  - » Kuwa mwangalifu kwa wanadoria wa usalama, walinzi wa kuvuka, baiskeli, na uwanja wa michezo.
- Angalia watoto kati ya magari na vitu vingine vilivyoegeshwa.



## Maeneo ya Ujenzi



- Maeneo ya kando ya barabara yataalamishwa na koni na pipa ya rangi ya machungwa inayong'aa.
  - » Endesha gari kwa uangalifu zaidi hadi ufkie ishara inayoonyesha mwisho wa eneo la ujenzi.
- Badilisha kasi ya kuendesha gari kwa kiasi kilichoonyeshwa.
  - » Punguza kasi hadi maili 45 kwa saa wakati wafanyakazi wapo.
- Adhabu za kuendesha kwa kasi ya juu au kufanya ajali katika eneo la ujenzi zinajumuisha:
  - » Faini mara mbili.
  - » Idadi kubwa ya pointi kwenye leseni ya kuendesha gari.
  - » Uwezekano wa kufungwa jela.
- Kuwa mwangalifu; maeneo ya ujenzi ni muhimu katika kuboresha barabara na kuzifanya kuwa salama.



## Njia za Kusafiri

- Magari yanapaswa kusafiri katika barabara ya upande wa kulia ikiwa barabara ina njia mbili au zaidi za kusafiri katika mwelekeo mmoja.
  - » Vighairi ni wakati unapita gari lingine.

## Ukiukaji wa Sheria za Kuendesha Gari



- Wamiliki wa leseni ya kuendesha gari wanawajibika kwa ada zote, faini, vikwazo, sheria, na utekelezaji wa sheria za Michigan.
- Kushindwa kulipa faini na ada au kukosa kwenda mahakamani kunaweza kusababisha leseni kusitishwa pamoja na gharama na adhabu za ziada.
- Sababu ya ukiukaji kwa kawaida itaorodheshwa kwenye tiketi.

## Dhamana ya Ukiukaji wa Trafiki



- Madereva wanapaswa bado kulipa tiketi au kuhuduria mahakama.
  - » Ikiwa unahuduria mahakama ndani ya siku 10, dhamana itatumika kuwadia faini na gharama za mahakama, na dhamana iliyobaki itarejeshwa.
  - » Ikiwa malipo yamewasilishwa kwa njia ya barua pepe, dhamana itarudishwa.
- Leseni za kuendesha gari zilizositishwa zitarejeshwa wakati wa malipo ya tiketi au kuonekana mahakamani.
  - » Tiketi itaandikiwa ili kuonyesha leseni ya kuendesha gari iliyositishwa.
  - » Tiketi haizingatiwi kuwa leseni ya kuendesha gari. Tiketi zinapaswa kulipwa haraka iwezekanavyo ili kuepuka kuendesha gari bila leseni halali.

## Kusimamishwa



- Cha kufanya wakati unapoona taa za dharura nyuma yako:
  - » Simama upande wa kulia wa barabara.
  - » Tulia na usubiri afisa.
- Cha kufanya wakati umesimama:
  - » Salia ndani ya gari lako.
  - » Weka mikono yote kwenye usukani.
  - » Waulize abiria kuweka mikono yao wazi.
- Jinsi ya kuongea na afisa:
  - » Ongea kwa upole.
  - » Toa leseni yako ya kuendesha gari, usajili wa gari, na ushahidi wa bima.
  - » USITOE au kupea afisa pesa.
  - » Ukiulizwa, toka ndani ya gari.
- Fahamu haki zako:
  - » Ikiwa unahisi haufai tiketi, unaweza kupinga mahakamani. Usilalamike kuhusu tiketi wakati umesimamishwa na maafisa wa trafiki.
  - » Wasiliana na msimamizi baada ya kusimamishwa na maafisa wa trafiki ikiwa unahisi hatua za afisa hazikuwa zinatafaa.
- Cha kufanya baada ya kusimamishwa:
  - » Funga mkanda wako wa usalama.
  - » Hakikisha ni salama kuingia tena barabarani.
  - » Tumia ishara yako ya kugeuka unapoingia tena kwenye barabara.



# Maelezo ya Usimamizi

# Usajili na Bima ya Gari



- Magari yanapaswa kusajiliwa kisheria Michigan, jimbo lingine, au nchi unayoishi.
- Magari yaliyoendeshwa Michigan kwa zaidi ya siku 90 mtawalia lazima yaandikishwe Michigan.
- Uthibitisho wa bima halali ya gari unaweza kutolewa kwa polisi kwa njia ya karatasi au kielektroniki, kama vile kwenye simu ya mkononi.
  - » Polisi wanaweza kuomba nakala ya elektroniki kutumwa kwao ili kuthibitishwa.
- Wamiliki wa gari wanapaswa kununua bima ya Michigan isiyo na dosari kabla ya kusajili gari lao. Sera za bima za nje ya jimbo hazikubaliwi.
  - » Bima ya uharibifu wa gari na wizi wa gari haihitajiki, lakini zinapendekezwa.

## Cheti cha Gari na Kuandikisha Gari

Unaponunua gari kutoka kwa  
mtu binafsi

Nunua gari

Katika Michigan, unaweza kuendesha gari lako mpya moja kwa moja hadi nyumbani bila nambari ya leseni, mradi ni ndani ya siku tatu za ununuzi.

Pata bima ya gari lako jipya

Leta cheti na uthibitisho wa bima  
kwenye ofisi ya Waziri ili kupata  
usajili, nambari, na nembo kwa  
gari mpya

Ni bora ikiwa wewe NA muuzaji mtaenda  
kwenye ofisi ya Waziri ili kukamilisha  
kubadilisha cheti.

Unaponunua gari kutoka kwa  
wauza magari

Muuzaaji atawea:

Kushughulikia makaratasi yote  
ya cheti, usajili, na nambari

Kukupa umenuna na kuwasilisha  
ushahidi wa Bima ya Michigan isiyo na  
dosari.

Kukusanya ada na kodi  
zinazohitajika

Kukupa nakala zote za nyaraka

## Leseni ya Michigan ya Kuendesha Gari



- Madereva wenyewe leseni lazima wawe wakazi wa Michigan na raia wa Marekani au wawe na kibali cha kisheria cha kuishi kwa kabisa au kwa muda mfupi.
  - » Makazi ina maana kuwa unaishi Michigan na umerhusiwa kisheria katika jimbo.
- Leseni halali ya dereva au kadi ya utambulisho ya jimbo kutoka nchi nyingine au Canada inaweza kutumika hadi upate makazi.
- Madereva wenyewe umri wa miaka 17 na chini hupewa leseni chini ya mpango wa Michigan wa Dereva Aliyehitimu Kupata Leseni isipokuwa wawe wamepata leseni katika jimbo lingine kwa zaidi ya mwaka mmoja.



## Leseni ya Mgeni ya Kuendesha Gari

- Watu wasio wakazi kutoka nchi fulani wanaweza kuendesha gari Michigan kwa kutumia leseni halali ya dereva. Chagua nchi zilizoodhereshwa hapa chini. Kwa orodha kamili tembelea Michigan.gov/SOS.
- Watu wasio wakazi wenye leseni halali ya kuendesha gari kutoka nchi zingine zote wanaweza kuendesha gari huko Michigan ikiwa:
  - » Hawalipwi au kufidiwa kwa kuendesha gari.
  - » Wanastahili kisheria kuwa Marekani.
  - » Wanabeba leseni ya kuendesha gari yenye tafsiri ya Kiingereza, Kibali cha Kimataifa cha Kuendesha gari, au hati husika.

Nchi	Endesha Gari kwa kutumia Leseni Halali	Endesha Gari ya Kibiashara kwa kutumia Leseni Halali ya Kibiahara
Brazili	Ndiyo	Ndiyo
Kolombia	Ndiyo	Ndiyo
Kostarika	Ndiyo	Ndiyo
Elsavado	Ndiyo	Ndiyo
Gwatemala	Ndiyo	La
Haiti	Ndiyo	La
Hondurasi	Ndiyo	Ndiyo
Jamaika	Ndiyo	La
Meksiko	Ndiyo	Ndiyo
Nikaragwa	Ndiyo	Ndiyo
Panama	Ndiyo	Ndiyo
Urugwai	Ndiyo	Ndiyo



Mwongozo huu ultengenezwa na Polisi wa Jimbo la Michigan,  
Divisheni ya Ruzuku na Huduma za Jamii, 2018.